OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA

SHULE YA SEKONDARI MWISENGE
S.L.P.1036,
MUSOMA

Tarehe……

Kumb Na…….

Jina la Mwanafunzi……
S.L.P…….

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWISENGE MANISPAA YA MUSOMA - MKOA WA MARA MWAKA 2021

- **UTANGULIZI.**

  Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika Shule hii **mwaka 2021**. Shule ya Sekondari Mwisenge ipo umbali wa **km 2** Magharibi mwa Halmashauri ya **Manispaa ya MUSOMA**.
  Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** saa moja Asubuhi, na mwisho wa kuripoti ni tarehe **28/02/2021.**

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA
2.1 SARE YA SHULE
A. WAVULANA

- Suruari 2 za rangi ya **Brown/ Udongo -ZISIWE ZA KUBANA MWILI (MODO HAZITAKIWI)**
- Shati 2 nyeupe mikono mifupi.
- Jozi za viatu vya ngozi vyeusi kisigino kifupi **(VYENYE KAMBA).**
- Soksi nyeupe jozi 2.
- Tai ndefu rangi ya **Brown/ Udongo** na
- Mkanda mweusi **(USIO NA UREMBO NA USIWE WA NAMNA YA UTAMBI)**
- Sweta rangi ya **Brown/ Udongo**

B. WASICHANA

- Sketi 2 ndefu na pana za rangi ya **Brown /Udongo** zenye marinda ya wastani **(ZIVUKE MAGOTI).**
- Shati 2 nyeupe za mikono mifupi **(ZISIWE ZA KUBANA)**
- Jozi ya viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi **(VYENYE KAMBA, VISIWE VIBAJAJI WALA RABA).**
- Soksi nyeupe jozi 2.
- Tai ndefu rangi ya **Brown/ Udongo**
- Sweta rangi ya **Brown/ Udongo**

C. RANGI YA HIJABU IFANANE NA SARE YA SHULE NA ISIWE YA KUBANA MWILI NA ISIWE NA UREMBO WA AINA YOYOTE

D. SARE YA MICHEZO KWA SHULE HII NI:

WAVULANA:

- Fulana 1 rangi ya **KIJANI KIBICHI**, Bukta 1 rangi ya bluu na Raba jozi 1.

WASICHANA:

- Fulana 1 rangi ya **KIJANI KIBICHI,** Bukta 1 PANA ya rangi ya bluu, na Raba jozi 1.

2.2 VIFAA VYA KITAALUMA

- Daftari kubwa 12(COUNTER BOOK QUIRE 3) na ndogo 12 za mazoezi.
- Kalamu rangi ya bluu/nyeusi za kutosha
- Rula 1 na pensel
- Mkebe wa hesabu 1(Mathematical set)
- Begi imara la kutunzia madaftari na **lisiwe la bobmarley**

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu **Na.25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria **Na.10** ya mwaka **1995**. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a)Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo lalazima;
b)Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima,
c) Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni saa 1:00 asubuhi kila siku za masomo
d)Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine atakazopewa;
e)Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa masomo.
f)Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule;
g)Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h)Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
i) Kutunza mali za umma.
j)**Mwanafunzi lazima aletwe na mzazi wake siku ya kuripoti shuleni.**

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi.
b) Uasherati na Ushoga.
c) Ubakaji.
d)Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito / kupata mimba.
i) Kutoa mimba.
j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
k)Kukataa adhabu kwa makusudi.
l) Kumiliki simu ya mkononi.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a)Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni.

b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA
……
MKUU WA SHULE
755833872/0655906022

REQUEST FOR MEDCAL EXAMINATION

PART A:

TO THE MEDICAL OFFICER

(Name in full) MR/MISS…….

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for enrolment as a secondary school student. The examination should include the following categories:-

- Eye sight…….
- Hearing……
- Limbs…….
- Speech…….
- Leprosy……
- Epilepsy…….
- Abdomen……
- TB…….
- Neurosis……..
- Pregnancy……

PART B:

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by government medical officer). I have examined the above named and consider that he/she is / is not physically fit and mentally fit for enrollment as a secondary school student.

- Eye sight…….
- Hearing……
- Limbs…….
- Speech…….
- Leprosy……
- Epilepsy…….
- Abdomen……
- TB…….
- Neurosis……..
- Pregnancy……

Name……Signature……Date……..……

Designation……

Station…….

Stemp…….

FOMU YA TAARIFA BANAFSI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI YA KUKUBALI SHERIA ZA SHULE

- **TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

  i)Jina kamili la mwanafunzi……

  ii)Tarehe ya kuzaliwa……..

  iii)mahali unapoishi (kata/kijiji/mtaa)……..

  iv)Uraia: Mtanzania / sio mtanzania……

  v)Shule aliyotoka ……..

  vi)Namba ya mtihani PS……

- **TAARIFA YA MZAZI/MLEZI**

  i)Jina la mzazi/mlezi……

  ii)Kazi ya mzazi/ mlezi……

  iii)Anwani ya mzazi/mlezi……

  iv)Simu ya mzazi /mlezi……

  (kama huna namba ya simu tumia ya ndugu/jirani yako) jaza taarifa katika jedwali lifuatalo:-

S/N	**JINA LA JAMAA/ NDUGU**	**NAMBA YA SIMU**	**ANAPOISHI**	**UHUSIANO**

- **AHADI YA MWANAFUNZI.**

  Mimi……..nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote ya kujiunga na shule ya sekondari……..na **nimekubali/sikubali** kuipokea nafasi niliyopewa. Ninaahidi kufuata na kutekeleza sheria na taratibu zote za shule, kusoma kwa bidii na niko tayari kupokea adhabu yeyote endapo nitavunja utaratibu wa shule kwa mkusudi.

  Sahihi…….

  Tarehe……..

- **AHADI YA MZAZI/MLEZI.**

  Mimi……Mzazi/mlezi wa mwanfunzi tajwa hapo juu **ninaahidi/siahidi** kushirikiana kwa karibu na uongozi wa shule katika malezi ya mwanangu. Pia nitampatia mwanangu mahitaji yote muhimu (fedha na vifaa kama uongozi wa shule ulivyoelekeza). Vilevile **niko/siko** tayari kupokea uamuzi utakaotolewa na uongozi wa shule endapo mwanangu atavunja **sheria na taratibu za shule** ikiwa ni pamoja na **kusimamishwa masomo, kupewa adhabu au kufukuzwa shule.**

  Sahihi ya Mzazi/Mlezi……

  Tarehe